## Amri ya Ulinzi ni nini?

Amri ya ulinzi ni amri ya mahakama ambayo inaweza kuwa zana ya kuongeza usalama kwa waathiriwa wa dhuluma za kinyumbani, dhuluma za kingono na kunyatia. Amri za ulinzi zinaweza kutolewa kwenye kesi ya raia au kama sehemu ya kesi ya uhalifu kwa uhalifu fulani unaohukumiwa.

Amri za ulinzi wa uhalifu hutumika tu wakati wa kesi ya kihalifu na zinaweza kuacha kutumika kwa ghafla bila onyo. Unaweza pia kutafuta Amri ya Ulinzi wa Mahakama iwe kuna kesi ya kihalifu au la. Amri za Ulinzi wa Mahakama zinaweza kuendelea kutumika hadi miaka mitano na zinaweza kusasishwa upya. Iwapo kuna kesi ya kihalifu inayosubiri kushughulikiwa, zungumza na mwanasheria kabla ya kuwasilisha madai ya kupata amri ya ulinzi wa mahaka kwa sababu hatua ya kuwasilisha madai ya kupata amri ya ulinzi wa mahakama inaweza kukuwacha bila ulinzi na inaweza kuathiri kesi ya uhalifu.

Kuna aina mbalimbali za amri za ulinzi wa raia zinazopatikana kulingana na uhusiano wako na mtu unayetaka kulindwa dhidi yake na aina ya dhuluma ambayo inatendeka au tayari imetendeka. Ili upate maelezo zaidi kuhusu aina za amri za ulinzi zinazopatikana, aina ambazo huenda unastahiki kupata na suluhu ambayo zinaweza kutoa, tembelea **www.odvn.org/survivor/law.html.**

## Je, Amri ya Ulinzi Inanifaa?

Hatari huongezeka mara nyingi pindi unapoanza kufikiria kuhusu na kuchukua hatua za kujitenga au kutamatisha uhusiano na mtu anayekunyanyasa. Amri za ulinzi zinaweza kukupa ulinzi kwa kiasi fulani, lakini hazikuhakikishii usalama. Hatua ya kuwasilisha madai ya kupata amri ya ulinzi inaweza pia kukusababishia matatizo mengine, hasa ikiwa: una watoto, una masuala mengine ya kisheria au una kesi nyingine ngumu kwa sababu nyinginezo. Ili upate maelezo zaidi kuhusu hatari za kujaza fomu ya kuomba amri ya ulinzi, tembelea **http://www.odvn.org/survivor/law.html** na ujaze orodha hakikishi ya "Je, Ninahitaji Kuwa na Mwanasheria Kwanza?"

Ni muhimi kubuni mpango wako mwenyewe wa usalama kwa msaada wa wakili wa dhuluma za kinyumbani. Unaweza kupata mpango wa karibu kwa kupiga simu kwa **800-934-9840**. Unaweza pia kuzungumza na wakili wa dhuluma za kinyumbani ili kugundua iwapo amri ya ulinzi ni uamuzi bora kwako. Hatua ya kuwasilisha ombi la kupata amri ya ulinzi bila ya kuwa na mpango wa usalama na ushauri wa kisheria huenda ikakufanya usiwe salama na inaweza kuongeza hatari kwako.

**odvn.org | 800-934-9840**

## Jinsi ya Kupata Usaidizi wa Kisheria

Katika hali nyingi, hasa iwapo una watoto au mali inayoshirikiwa au deni na mtu anayekudhulumu, ni muhimu zaidi kupata mwanasheria kabla ya kuwasilisha madai. Zifuatazo ni njia za kujaribu kupata mwanasheria na maelezo ya kisheria:

- **Ofisi za Usaidizi wa Kisheria:** Piga simu kwa **866-lawohio (866-529-6446)** au nenda kwa: **www.ohiolegalhelp.org** ili upate ofisi ya usaidizi wa kisheria ya jumuiya yako. Wanaweza kukupa mwanasheria bila malipo.
- **Mipango ya Dhuluma za Kinyumbani:** Kuna mipango inayopatikana kwa waathiriwa ambao wanahitaji amri za ulinzi ambayo inaweza kukupa huduma za kisheria bila malipo bila kuzingatia kipato chako. Wakili wako wa eneo anapaswa kuweza kukuunganisha na mipango hii na Mpango wa Fidia kwa Waathiriwa wa Uhalifu.
- **Wanasheria wa Kujitolea/Wasiolipwa:** Baadhi ya jumuiya zina wanasheria wa kujitolea. Iwapo wakili wako hawezi kukuunganisha na mwanasheria wa kuaminika, unaweza kuwasiliana na Muungano wa Mawakili wa Kulipwa wa eneo lako kuona iwapo mwanasheria wa kujitolea anaweza kukusaidia. Iwapo kuna chuo cha sheria karibu na mahali unakoishi, angalia iwapo wana usaidizi wa kisheria usiolipishwa kupitia kliniki ya kisheria.

Ni mwanasheria pekee ndiye anayeweza kukupa ushauri wa kisheria au kukusaidia kuwasilisha kesi yako mahakamani. Wakili anaweza kukusaidia kutengeneza mpango wa usalama unaokufaa zaidi, ambayo ni sehemu muhimu ya hatua yoyote ya kisheria unayochukua.

Ohio Domestic Violence Network ODVN

The Ohio Domestic Violence Network (ODVN is a statewide coalition of domestic violence programs, supportive agencies, and concerned individuals working together to stop domestic violence through education, information and training for those who are affected by domestic violence, and by promoting social and systems change.

This project is supported by Grant No. G-1901OHSDVC awarded by the Department of Health & Human Services, Administration for Children and Families (ACF), Administration on Children, Youth, and Families (ACYF), Family and Youth Services Bureau (FYSB). The opinions, findings, conclusions, and recommendations expressed in this publication, program, exhibition are those of the author and do not necessarily reflect the views of the Department of Health & Human Services.

SWAHILI CPO BROCHURE

# AMRI YA ULINZI NI NINI?



Ohio Domestic Violence Network ODVN

## Ninawezaje Kutafuta Amri ya ulinzi?

Mchakato hutofautiana katika kila nchi. Wasiliana na mpango wa dhuluma za kinyumbani wa eneo lako ili kupata maelezo kuhusu jinsi mchakato hufanya kazi katika nchi yako. Wanaweza pia kukusaidia katika kuwasilisha madai yako ya ombi la kupata amri ya ulinzi au kukusaidia kupata mwanasheria. Huhitaji mwanasheria ili kuwasilisha madai ya kupata Amri ya Ulinzi, lakini huenda mchakato ukawa na changamoto na ni vyema kuwa na mwanasheria kila wakati. Ni muhimu hasa kuzungumza na mwanasheria kabla ya kuwasilisha madai ya iwapo umepata watoto na mtu anayekunyanyasa au una masuala mengine ya kisheria. Unaweza kupata mwanasheria bila malipo kupitia usaidizi wa kisheria wa eneo lako, Mpango wa Fidia kwa Waathiriwa wa Uhalifu au mpango mwingine wa wanasheria wasiolipwa (bila malipo). Unaweza kupata hati za kuwasilisha madai ya kupata amri ya ulinzi kutoka kwa karani wa mahakama katika jimbo ambalo utakuwa unawasilisha madai. Unaweza pia kupakua fomu kutoka kwa tovuti ya Mahakama ya Juu ya Ohio (**www.supremecourt.ohio.gov/JCS/domesticViolence/default.asp**). Iwapo unatumia tovuti zozote katika mchakato wako, hakikisha kuwa unatumia kompyuta ambayo haiwezi kufikiwa na mtu anayekunyanyasa, kama vile kompyuta ya rafiki unayemwamini au ya maktaba.

## Je, Mchakato wa Mahakama Hufanya Kazi Vipi?

**Hatua ya 1: UWASILISHAJI MADAI–**Mwathiriwa au mwanasheria wake huwasilisha ombi la amri ya ulinzi. Iwapo unahitaji ulinzi wa papo hapo, ombi linapaswa kujumuisha ombi kuwa mahakama itekeleze shughuli ya kusikiliza upande mmoja pekee.

**Hatua ya 2: KUSIKILIZA UPANDE MMOJA PEKEE–**Mahakama hutekeleza shughuli ya kusiklizа upande mmoja pekee (inamaanisha kuwa kuna mshirika mmoja pekee) katika kipindi fulani cha muda kinachohitajika kisheria. Kwa CPO, ni siku sawa na ya kuwasilisha madai. Kwa Amri ya Ulinzi dhidi ya Kunyatia na/au Kosa Linalohusiana na Ngono (SSOOPO) au Amri ya Ulinzi wa Watoto, hutekelezwa siku iyo hiyo au siku inayofuata ya kikao cha mahakama baada ya kuwasilisha. Hii ni fursa yako ya kumweleza jaji kwa nini unahitaji amri ya ulinzi wa mara moja na jaji ataamua iwapo atatoa au hatatoa amri siku hiyo.

**Hatua ya 3: KUTOLEWA KWA HATI–**Mshtakiwa (mtu uliyewasilisha ombi la ulinzi dhidi yake) hupewa nakala ya madai uliyowasilisha, Amri ya Ulinzi (iwapo illitolewa wakati wa kusikiliza upande mmoja pekee) na ilani ya kikao kamili cha mahakama. Huu unaweza kuwa wakati hatari zaidi na mpango wako wa usalama unapaswa kuangazia mahitaji yako ya ziada ya usalama katika kipindi hiki.

**Hatua ya 4: KIKAO KAMILI CHA MAHAKAMA–**Mahakama huwa na kikao kamili kwa kawaida ndani ya siku 7-10, ambacho ni lazima uhudhurie. Jambo lolote kati ya yafuatayo linaweza kutendeka: huenda kikao kikaahirishwa hadi tarehe nyingine, wewe na mshtakiwa mnaweza kufikia makubaliano ya kutolewa kwa amri ya ulinzi ambayo hujulikana kama Makubaliano ya Idhini au huenda kukawa na kikao cha mahakama.

- **Unapaswa kuwa tayari kuendelea kuhudhuria kikao cha mahakama kwa tarehe yoyote ambayo imewekwa ya kikao cha mahakama pamoja na shahidi, ushahidi na kitu chochote ambacho uliwasilisha katika ombi lako. Huenda mahakama pia ikaruhusu kuwasilishwa kwa maelezo mengine kuhusu malezi na kumtembelea mtoto wako, matumizi ya dawa, hali za makazi n.k.**

**Hatua ya 5: AMRI ZA MAHAKAMA–**Huenda mahakama ikatoa amri wakati wa kikao cha mahakama au huenda ikasubiri kutoa amri ambayo utatumiwa kwenye barua pepe. Huenda amri zikawa na nguvu – ikiwa ni pamoja na ambapo Mshtakiwa anaweza kuwa, yeye ndiye anayepewa ulezi wa mtoto, anayeweza kuishi katika nyumba na iwapo Mshtakiwa anaweza kuwa na uwezo wa kufikia bunduki. Huenda pia amri ya mahakama ikakosa kutoa amri ya ulinzi na kufanya iwe vigumu zaidi kwako kuwa salama siku za baadaye.

**Endelea kuhifadhi amri yako ya ulinzi kila wakati katika hali ambapo huenda utahitaji kupiga simu kwa polisi ili kuitekeleza. Toa nakala za amri kwa watu wengine ambao huenda wakazihitaji, kama vile shule ya mtoto wako au kazini kwako.**

## Kujitayarisha Kuhudhuria Mahakama Kabla ya Kikao chako cha Mahakama

- Fahamu jinsi ya kufika mahakamani na kuegesha (iwapo inahitajika). Panga kufika mapema kwa kikao chochote cha mahakama.
- Ni muhimu kuwa msafi na nadhifu mahakamani.
- Fanya mipango ya awali na wakili na mwanasheria wako kuhusu mahali ambapo unaweza kusubiri ili usiweze kukutana na mshtakiwa kabla, wakati au baada ya mahakama. Tafuta usaidizi kutoka kwa wafanyakazi wa mahakama iwapo mshtakiwa atajaribu kukufikia kwa njia yoyote isiyoruhusiwa au iwapo unahitaji mlinzi ili kuondoka.
- sipokuwa iwapo watoto wako watatoa ushahidi, si wazo nzuri kuwaleta mahakamani. Weka mipango ya huduma ya utunzi wa watoto kabla ya kuhudhuria mahakama huku ukifahamu kuwa kikao cha mahakama huenda kikachukua muda mrefu au mfupi wa siku. Mwelezee wakili wako iwapo huwezi kupata huduma za utunzi wa watoto.
- Soma na uwe na ufahamu kuhusu madai uliyowasilisha na ushahidi wako kabla ya kuhudhiria kila kikao cha mahakama. Hakikisha kuwa mashahidi wako wanapatikana na watoe hati ya kuitwa mahakamani iwapo wanahitajika.
- Una haki ya kisheria ya kuandamana na wakili mahakamani kwa vikao vyako vyote vya mahakama.
- Una haki ya kupata mkalimani anayetolewa na mahakama iwapo huzungumzi Kiingereza au iwapo wewe ni kiziwi au una matatizo ya kusikia. Ifahamishe mahakama au wakili wako iwapo unahitaji mkalimani wakati unapowasilisha madai na wakati wowote ambao kikao cha mahakama kimewekwa. Ni vizuri kuwa na mwanasheria kwa vikao hivi vya mahakama kila wakati.

## Vidokezo vya Kutoa Ushahidi

- Zingatia ukweli na ujibu maswali unayoulizwa pekee. Iwapo unahitaji kutoa maelezo zaidi, huenda ukahitaji kusubiri zamu yako ya kuzungumza tena.
- Zungumza kwa sauti na uwazi ili jaji na mtangazaji wa mahakama waweze kukusikia.
- Epuka kutumia maneno yoyote, kama vile lugha ya kisheria na matibabu, iwapo hujui maana yake.
- Chukua muda wako wakati wa kujibu maswali. Iwapo huelewi swali au hujui jibu lake, sema. Usijibu swali lolote hadi uelewe kikamilifu unachoulizwa.
- Kuwa makini mahakamani na umrejelee jaji kila wakati kama "Mheshimiwa."
- Mshtakiwa au mwanasheria wa Mshtakiwa huenda akasema mambo yanayokasirisha au huenda hata akajaribu kukutia hasiria. Zingatia kuwa mtulivu. Mwombe jaji muda wa mapumziko iwapo unauhitaji.

## Itakuwaje iwapo Amri Yangu ya Ulinzi Itakiukwa?

Amri yako ya ulinzi itatekelezwa kila mahali unapoenda Marekani. Iwapo amri yako ya ulinzi itakiukwa, zungumza na wakili ili kubadilisha mpango wako wa usalama. Unaweza pia:

- Kukusanya na kuhifadhi ushahidi wowote. Hii inaweza kujumuisha kupiga picha za mnyanyasaji, gari lake au uharibifu wa mali uliofanywa au kuhifadhi ujumbe au ujumbe wa simu, machapisho ya mitandao ya kijamii au barua pepe.
- Piga simu kwa polisi na uwaombe kutekeleza amri yako ya ulinzi (kwa kumkamata mshtakiwa). Hatua ya kukiuka amri ya ulinzi inaweza kuwa kosa la kihalifu. Iwapo utawapigia simu polisi, fanya hivyo haraka iwezekanavyo wakati au baada ya ukiukaji. Iwapo hawatamkamata, waombe kuandikisha ripoti.
- Zungumza na kiongozi wa mashtaka ambapo amri yako ilikiukwa kuhusu uwasilishaji wa madai ya kihalifu.
- Wasilisha mjadala ili mshtakiwa ahukumiwe kwa kukiuka amri ya mahakama katika mahakama halisi ambayo ilitoa amri yako ya ulinz.

Ohio Domestic Violence Network
ODVN

**odvn.org | 800-934-9840**